JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

No. 16 of 1990

NAKUBALI,

..........................................
*Rais*

..........24/9/90..........

**Sheria ya kufanya mabadiliko katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuweka masharti mapya ya uteuzi wa mgombea pekee katika uchaguzi wa Rais wa Zanzibar**

[ ........................................ ]

SHERIA HII imetungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Jina la Sheria

**1.** Sheria hii iitwe Sheria ya Mabadiliko ya Saba ya Katiba ya Nchi, ya mwaka 1990.

Kufanya mabadiliko katika ibara ya 104

**2.** Ibara ya 104 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya mwaka 1977, inafanyiwa mabadiliko kwa kuifuta ibara ndogo ya (3), ya (4) na ya (5) za ibara hiyo na badala yake kutakuwa na masharti mapya yafuatayo:

> "(3) Wakati wa kumchagua Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ukiwadia, Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa itakutana, na kwa mujibu wa masharti ya Katiba ya Chama itatoa pendekezo la jina la mtu mmoja kutoka Tanzania Zanzibar, aliyetimiza umri usiopungua miaka arobaini, mwenye sifa za kusimama kama mgombea pekee katika uchaguzi wa Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
>
> (4) Jina la mtu huyo aliyependekezwa katika uteuzi wa mwanzo uliofanywa na Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (3) litawasilishwa kwenye Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama ambayo nayo itakutana na kufanya uteuzi wa mwisho wa mtu atakayesimama katika uchaguzi wa Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mujibu wa masharti ya ibara hii.

(5) Huyo mtu aliyeteuliwa katika uteuzi wa mwisho na Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama kugombea kiti, atasimama katika uchaguzi, na wananchi watapiga kura ya kumkubali au kumkataa, na kwa kutegemea matokeo ya kura hiyo, mambo yatakuwa ifuatavyo:—

(a) ikiwa zaidi ya nusu ya wapiga kura wote wamemkubali mgombea kiti, basi mtu huyo atakuwa amechaguliwa kuwa Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar itamtangaza kuwa amechaguliwa;

(b) ikiwa zaidi ya nusu ya wapiga kura wote wamemkataa mgombea kiti, basi mtu huyo atakuwa hakuchaguliwa kuwa Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na katika hali hiyo Kamati Maalum ya Kamati Kuu ya Chama itakutana tena na kupendekeza jina la mtu mwingine, na Halmashauri Kuu ya Taifa yaChama, halikadhalika, itakutana tena na kufanya uteuzi wa mwisho, kama ilivyoelezwa katika ibara ndogo ya (4), na hatimaye uchaguzi utafanywa kwa mujibu wa ibara hii ndogo".

Passed in the National Assembly on the twentieth day of July, 1990.

*Clerk of the National Assembly*

Printed by the Government Printer, Dar es Salaam, Tanzania